

CIRCULAR

MAJAJI WOTE WA MAHKAMA KUU

MTENDAJI MKUU WA MAHKAMA

KADHI MKUU, NAIBU KADHI MKUU, KADHI WA RUFAA

MRAJIS/NAIBU WARAJIS

MAHAKIMU WOTE

MAKADHI WOTE

WAFANYAKAZI WOTE WA MAHKAMA

**HATUA ZA KIUTAWALA NA DHARURA ZA KUKINGA NA KUPUNGUZA
MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA (COVID 19) KWA MAHKAMA**

Kufuatia maelekezo yaliyotolewa na Serikali ya Zanzibar tarehe 17 Machi, 2020 juu ya kujikinga na kupunguza kuenea kwa virusi vya corona (COVID- 19) hapa Zanzibar, natoa muongozo ufuatao katika uendeshaji wa kesi Zanzibar.

1. Usikilizwaji wa kesi zote unasitishwa kwa muda wa siku 30 kuanzia tarehe 26 Machi, 2020 hadi tarehe 24, April, 2020. Kwa zile kesi ambazo ziko katika hatua ya 'submission', Mahkama husika itawashauri Mawakili au wenye kesi kuwasilisha kwa maandishi.
2. Mahkama zitashughulikia kesi za dharura na kwa washtakiwa wenye kesi nzito na maombi ya dhamana. Muombaji na wakili wake au kwa ombi la dhamana wadhamini ndio watakaoruhusiwa kuingia Mahkamani.
3. Kwa makosa yenye dhamana, Majaji na Mahakimu wanatakiwa kutoa dhamana yenye masharti nafuu ili kupunguza mrundikano katika Chuo cha Mafunzo kwa kipindi hichi.
4. Katika kipindi hichi, watendaji wote wa Mahkama wataendelea kuwepo kazini. Hata hivyo, Kumbi za Mahkama (Open Court) hazitatumika. Kwa

Majaji na Mahakimu wenye Hukumu na Maamuzi (Ruling) watatumia kipindi hichi katika kuzikamilisha.

5. Zaidi ya muongozo uliotolewa hapo juu 'sanitizers'. na hatua nyengine za kinga zinawekwa.

Muongozo huu unaweza kurekebishwa wakati wowote kufuatana na maelekezo yatakayotolewa na Serikali.



OMAR O. MAKUNGU
JAJI MKUU